## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

**Tarehe: 28.03.2024**

### TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anapenda kuwajulisha wananchi wote kuwa, hadi sasa Serikali haijatoa utaratibu wa utoaji wa mikopo ya asilimia Kumi kupitia Vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu.

Hivyo, tahadhari inatolewa kwa umma kujiepusha na baadhi ya watu wanaopita kwa watu binafsi au vikundi kwa lengo la kuwashawishi watoe fedha ili wasaidiwe kupata mikopo.

Endapo utakutana na Mtu anakushawishi kutoa fedha ili kukusaidia kupata mkopo, tafadhali toa taarifa Ofisi ya Mkuu wa wilaya, Ofisi Mkurugenzi wa Manispaa kwa kupiga simu na. 0733241052 ili hatua za kisheria zichukulıwe haraka.

Aquilinus Shiduki
MGCO
**Manispaa ya Kinondoni**

*Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Manispaa ya Kinondoni, S.L.P. 31902, 2 Barabara ya Morogoro, 14883 Dar es Salaam,*
*Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu: +255 2170173 Nukushi: 2172606, Barua pepe – md@kinondonimc.go.tz*